# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya
Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA YA HABARI, SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,**

Kwanza kabisa hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuamsha salama leo hii na kutuwezesha kufika hapa kwa lengo la kulitumikia taifa na wananchi wake.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda pia kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi zake katika kutekeleza vyema vipaumbele vya vya Sekta ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo kwa vitendo. Wananchi wanashuhudia maendeleo makubwa katika Sekta hizi mijini na vijijini kwa kipindi cha uongozi wake. Tunamuomba Allah amzidishie Rais wetu hekima na uadilifu katika kuingoza nchi na wananchi wake wote bila ya kuangalia tofauti zao za kiitikadi, kidini na kikabila.

**Mheshimiwa Spika,**

Nachukuwa nafasi hii pia kumshukuru Mhe. Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo pamoja na watendaji wake wote kwa juhudi zao katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa kazi nzuri wanazozifanya. Muda wote wa Kamati wamejaribu kuonesha umahiri na weledi wao katika kuchanganua na kujadili ipasavyo Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara na hatimae kuishauri vyema Serikali na Wizara, ili fedha itakayoidhinishwa na Baraza lako tukufu, iweze kutumika kama ilivyotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo:

1. Mheshimiwa Hussein Ibrahim Makungu — Mwenyekiti
2. Mheshimiwa Dkt. Nasra Nassor Omar — M/Mwenyekiti
3. Mheshimiwa Issa Haji Ussi Haji (Gavu) — Mjumbe
4. Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub — Mjumbe
5. Mheshimiwa Seif Hamad Suleiman — Mjumbe
6. Mheshimiwa Shaame Ali Ali — Mjumbe
7. Mheshimiwa Zainab Khamis Shomari — Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati hii pia inafanyakazi kazi zake kwa kusaidiwa na Makatibu wafuatao:

1. Ndugu Mwaka Mwinyi Waziri
2. Ndugu Mussa Issa Mussa
3. Ndugu Mohamed Rymond Mwellu (Afisa Bajeti)

**Mheshimiwa Spika,**

Moja kati ya jukumu la Msingi la Kamati hii ni kupitia, kuyachambu na

kuyajadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa kila mwaka wa fedha, kama Kanuni ya 101 (2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2024 inavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu ilikaa kuyapitia na kuyajadili Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo na kutoa Maoni na Ushauri kwa yale mapungufu ambayo yamejitokeza katika utekelezaji wa shughuli kwa mwaka uliopita na kwa yale ambayo yanaweza kukwamisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka mpya wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Habari ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi **milioni 710,000,000** na hadi kufikia Machi 2026 Wizara ilifanikiwa kukusanya shilingi **milioni 318, 437,250** sawa na asilimia 45 ya Makadirio ya mwaka, ambapo jumla ya shilingi **milioni 581,500,000** zimekadiriwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2026/2027, fedha ambayo imepungua kulinganisha na Makadirio kwa mwaka uliopita.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo kusimamia kwa karibu vyanzo vyake vya mapato, ili waweze kufikia lengo la ukusanyaji lililokadiriwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka huu wa fedha 2026/2027 Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo imepanga kutekeleza majukumu yake kupitia Programu kuu tatu, ambazo ni Programu Kuu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji, Programu Kuu ya Utamaduni, Sanaa, Ubunifu na Michezo na Programu Kuu ya Uongozi na Utawala. Jumla ya shilingi **bilioni 243,352,740,000** zimekadiriwa kutumika kwa Matumizi ya Kawaida pamoja

na Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kupitia Programu hizi Kamati imebaini baadhi ya changamoto kadhaa ambazo kuendelea kuwepo katika Makadirio haya kunaweza kuathiri utekelezaji wa majukumu kwa Taasisi zilizomo ndani ya Wizara hii na matokeo chanya hayatoweza kufikiwa.

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA HABARI, SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii inalengo la kuhakikisha kuwa Utamaduni, Lugha ya Kiswahili na Sanaa Zanzibar zinaenziwa na wasanii wanaendelezwa kiuchumi ili kupunguza umasikini na kufanya michezo kuwa sehemu ya kujenga amani, utulivu, ajira pamoja na kujenga afya kwa jamii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imebaini baadhi ya taasisi, kupangiwa kukusanya Mapato makubwa ukilinganisha na vyanzo walivyonavyo, hali inayowapa wakati mgumu watendaji katika kutekeleza majukumu yao. Mfano mzuri ni Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA).

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 BAKIZA ilipangiwa kukusanya

Jumla ya shilingi Milioni 50,000,000 na hadi kufikia mwezi Machi 2026 BAKIZA ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi Milioni 10,933,500 tu sawa na asilimia 22%, ya makadirio ya mwaka, kupitia uuzaji wa vitabu na Majarida ya Kiswahili, Kongamano la Kimataifa na kutoa mafunzo mafupi kwa walimu wanaowafundisha wageni lugha ya Kiswahili.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, BAKIZA imepangiwa kukusanya mapato ya jumla ya shilingi Milioni 35,000,000 na kupanga kutumia jumla ya shilingi Milioni 700,340,000. Kupitia hali hii, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuwaingizia BAKIZA fedha yote iliyokadiriwa, ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ya kukikuza, kukieneza na kukiendeleza Kiswahili ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande mwengine, Kamati imebaini changamoto ya ufinyu wa ofisi pamoja na ukosefu wa usafiri kwa Baraza la Kiswahili Zanzibar. (BAKIZA). Ufinyu wa ofisi inayotumiwa na Baraza hili, unatoa taswira mbaya kwa watendaji na wageni wanaofika katika taasisi hiyo kwa lengo la kupata taaluma. Tukumbuke kwamba Ofisi hii ni muhimu hasa tukizingatia wageni wengi kutoka ndani na nje ya nchi hufika kwa lengo la kujipatia taaluma inayohusu lugha ya Kiswahili.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mnasaba huu, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo kuipatia BAKIZA ofisi itakayokuwa na mazingira mazuri ya kiutendaji kwa wafanyakazi. Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuwatafutia usafiri wa uhakika ili kuondokana na changamoto hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imebaini kwamba, fedha nyingi iliyokadiriwa kwa utekelezaji wa Programu hii ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo imeegemea zaidi katika Program Ndogo ya Uendelezaji wa Utamaduni, Sanaa, Ubunifu na Michezo lakini malengo ya Wizara hayaoneshi kwa uwazi jinsi ya utekelezaji wa moja kwa moja wa Sanaa na ubunifu katika Wizara. Jumla

ya shilingi **bilioni 227,760,808,000** zimekadiriwa kutumika kwa Programu hii ya Maendeleo ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **16,902,678,000** zinatarajiwa kutumika kwa Program Ndogo ya Uendelezaji wa Utamaduni, Sanaa, Ubunifu na Michezo.

## PROGRAMU YA HABARI UTANGAZAJI NA UCHAPAJI

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii inalenga kuongeza upatikanaji na usambazaji wa habari sahihi na kwa wakati kwa wananchi kupitia vyombo vya habari. Programu hii inatekelezwa kupitia Programu ndogo mbili ambazo ni Programu Ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari na Programu Ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari na Utangazaji na Uchapaji. Kwa mwaka wa Fedha 2026/2027 Programu hizi zimekadiriwa kutumia jumla ya shilingi **bilioni 7,980,893,000.**

**Mheshimiwa Spika,**

Shirika la Utangazaji Zanzibar ni nguzo muhimu katika kulifikia lengo hili. Kamati imeridhika na utekelezaji wa shughuli za Shirika hili kwa kuipasha jamii taarifa zilizo sahihi na wakati muafaka.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kuboresha huduma za utoaji wa taarifa kwa Shirika letu, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo kulifanyia ukarabati jengo la kituo cha Utangazaji Mkanjuni Pemba, ambalo kwa sasa haliko katika hali nzuri. Kituo kinapaswa kuwekwa vifaa vya kisasa vyenye ubora unaoendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Aidha, kuongeza idadi ya wafanyakazi pamoja na idadi ya vipindi vitakavyonekana moja kwa moja (Live), hii itasaidia sana kuongeza idadi ya hadhira pamoja na mapato kwa Shirika hili.

**Mheshimiwa Spika,**

Shirika la Utangazaji limekadiriwa kutumia jumla ya shilingi bilioni **3,502,756,000** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuingizia fedha hii kwa wakati, ili Shirika letu liweze kupiga hatua katika kuendeleza sekta ya habari nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, Kamati inaipongeza kwa dhati Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wake Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi kwa kuimarisha sekta ya michezo nchini ambapo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imegharamia fedha zote za Mradi wa ujenzi wa Mji wa Michezo katika eneo la Fumba kwa asilimia mia moja. Jumla ya USD 150,000,000 zimepangwa kutumika katika Mradi huu, ambapo hadi kufikia machi 2026 jumla ya dola za Kimarekani Milioni 34.0 sawa na aslilimia 22.6 zimetumika.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati pia inaipongeza Serikali kwa hatua nzuri iliyofikia ya ukarabati wa uwanja wa Gombani Pemba, uliojumuisha kazi mbalimbali zikiwemo za ujenzi wa uzio, ukarabati wa vyumba vya viongozi mashuhuri, vyumba vya kubadilishia nguo kwa wachezaji pamoja na maeneo ya mapokezi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo kuimarisha huduma za usafi katika uwanja huu, ili uweze kubakia katika ubora wake hasa tukizingatia fedha nyingi zilizotumika katika kuukarabati uwanja huo.

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho kabisa, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu, Maoni na Ushauri wa Kamati yangu kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya

Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Sasa niwaombe wajumbe wa Baraza lako tukufu kuijadili, kuichangia na kuiunga mkono bajeti hii, ili kumuwezesha Mheshimiwa Waziri kutekeleza majukumu ya Wizara yake kama alivyojipangia.

**Mheshimiwa Spika,**

Mimi binafsi na kwa niaba ya Kamati yangu ya Ustawi wa Jamii naiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

Naomba kuwasilisha,

Ahsante sana,

……………………

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu

Mwenyekiti,

Kamati ya Ustawi wa Jamii,

Baraza la Wawakilishi,

**<u>Zanzibar.</u>**